
MCHANGO WA KOMEDIA ZA KISWAHILI KATIKA UJIFUNZAJI WA

LUGHA YA KISWAHILI

Karuhanga Deusdedit

Metropolitan International University

IKISIRI

Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza mchango wa komedia za Kiswahili katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa Wanafunzi wa Chuo Kikuu Cha Kitaifa cha Metropolitan. Utafiti huu umejengeka kwa msingi kwamba fasihi yeyote kokote iwapo huchangia sana katika usambazaji na ujifunzaji wa lugha, lakini utanzu wa komedia hasa za Kiswahili, umeachiliwa nyuma na kuangaliwa kama utanzu duni katika ujifunzaji na usambazaji wa lugha ya Kiswahili. Badala yake, tanzu nyingine zimepewa nafasi ya kwanza na kusemwa kuwa ndizo zinazotoa mchango mkubwa katika ujifunzaji na usambazaji wa lugha ya Kiswahili. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya ueneaji ambayo inazingatia chimbuko la taaluma fulani na kujaribu kufuata mikondo iliyopitia hadi kufikia hali ilivyo wakati wa uchambuzi. Tasnifu hii iliongozwa na madhumuni matatu yafuatayo: kubainisha komedia mbalimbali zinazopendwa na Wanafunzi wa tarafa ya Biharwe ; kuchunguza mchango wa komedia zinazopendwa na Wanafunzi wa tarafa ya Biharwe katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili pamoja na changamoto mbalimbali zinazokumba utanzu wa komedia za Kiswahili katika uendelezaji na usambazaji wa lugha ya Kiswahili kwa Wanafunzi wa tarafa ya Biharwe jijini Mbarara. Utafiti huu ulilenga kujibu maswali yafuatayo: ni komedia zipi ambazo zinapendwa na Wanafunzi wa Chuo Kikuu Cha Kitaifa cha Metropolitan? komedia za Kiswahili zimechangiaje katika ujifunzaji na usambazaji wa lugha ya Kiswahili kwa Wanafunzi wa Biharwe? na utanzu wa komedia unakumbwa na changamoto zipi katika usambazaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa Wanafunzi wa Chuo Kikuu Cha Kitaifa cha Metropolitan jijini Mbarara. Data ya utafiti huu ilikusanywa kutoka nyanjani ambapo mtafiti alitumia maskani ya

wanafunzi wa Chuo Kikuu Metropolitan ambayo ni “White house ”, na “Altimate” yanayopatikana katika tarafa ya Biharwe jijini Mbarara. Data ya utafiti huu ilikusanywa kwa kutumia mbinu ya mahojiano, hojaji na majadiliano. Matokeo ya utafiti yalichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya maelezo yaliyolenga kufafanua majedwali na michoro iliyopatikana katika data yake. Utafiti huu uligundua kuwa kwamba Wanafunzi wengi wanazipenda komedia za Professa Hamo. Matokeo yalionyesha kuwa komedia za Kiswahili zinachangia pakubwa katika ujifunzaji na usambazaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa Wanafunzi wa tarafa ya Biharwe kwani zinawafunza wanajamii hasa Wanafunzi wa Biharwe misamiati mipya na jinsi ya kuizalisha misamiati hiyo, mtafiti aligundua kuwa uchanganyaji ndimi kama mbinu ya uwasilishaji huwafanya watazamaji kutoelewa baadhi ya mambo yanayozungumziwa na vile kuwafanya wasijifunze lugha ya Kiswahili kwa urahisi. Utafiti huu utoonyesha mchango wa komedia za Kiswahili katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Pia, utawasaidia watafiti wengine kwa kufanya kama nguzo ya kuwaongoza watakapokuwa wanatafiti jambo linalohusiana na mada hii. Mtafiti alipendekeza kwamba kuna haja ya kuanzisha uchezaji na utunzi wa komedi za Kiswahili nchini Uganda ili sanaa hii ifikie umati mkubwa wa wanajamii; kuna haja ya kuanzisha kuzionyesha hizi komedia za Kiswahili kenye vituo vya televisheni nchini Uganda ili ziweifike watu wengi na wajifunze lugha ya Kiswahili moja kwa moja na kwamba komedia za Kiswahili zafaa sana kuwekewa mashindano kwenye shule mbalimbali, vyuo na ndaki mbalimbali ili kuinua mapenzi ya wanajamii kuzihusu na kuhusu lugha ya Kiswahili na lengo la kuwafanya watoe imani potovu kuhusu kutofaa kwa lugha ya Kiswahili.

Usuli wa Mada

Utafiti huu unahusu mchango wa komedia za kiswahili katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa Wanafunzi wa Chuo Kikuu Cha Kitaifa cha Metropolitan jijini Mbarara. Sura hii inazingatia usuli wa mada, Tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, upeo wa utafiti, umuhimu wa utafiti pamoja na misingi ya nadharia ya utafiti.

Kwa mujibu wa Habwe na Karanja, (2004), lugha ni mfumo wa sauti zinazotumiwa na watu wa jamii wenye utamaduni unaofanana ili kuwasiliana. Lugha ni mfumo wa sauti nasibu na ishara za kisarufi ambazo kwazo watu wa jamii fulani ya lugha huwasiliana na kupokezana utamaduni wao. Hii ina maana kwamba lugha ni chombo muhimu cha utamaduni, lugha ni sehemu ya utamaduni na ni chombo kinachosheheni sifa za utamaduni wa jamii husika katika misamiati, miundo na matumizi ya lugha zinazohusika. Lugha hutumika kukuza utamaduni kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Kwa mujibu wa (TUKI, 2005), Lugha ni mpangilio wa sauti na maneno unaoleta maana ambayo hutumiwa na watu wa taifa au kundi Fulani kwa ajili ya kuwasiliana. Mahusiano ya kijamii hujengwa kutokana na historia, mazingira na shughuli za watu za kila siku na imani yao pia. Watu wa jamii moja mara nyingi husikilizana kwa lugha, mila na desturi. Misingi hiyo ya utamaduni na utamaduni wenyewe huwa ni vigezo maalum vya kumfanya mtu aitambue nafasi yake katika jamii na vilevile kutambua wajibu wake na majukumu yake, Mazrui (1986).

Tamthilia ni utungo wa kisanaa ambao huweka wazo fulani katika matendo na mazungumzo (TUKI, 2004). Hivyo basi tunaweza kusema kuwa tamthilia ni utungo au mchezo wa kuigiza matendo au mawazo fulani yaliyopo katika jamii, ambapo huwa ni majibizano baina ya watu wawili au zaidi.

Fasihi ni sanaa inayotumia lugha kwa njia ya ubunifu kuelezea masuala mbalimbali yanayomuhusu binadamu na mazingira anamoishi. Na fasihi hugawika katika aina kuu mbili ambazo ni fasihi andishi na fasihi simulizi. Bakhtin (1986) na King'ei (2000) wanakubaliana kuwa fasihi hukua, hubadilika na kuathirika kutokana na hali mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Hivyo, kazi yoyote ya fasihi inatazamiwa kubadilika wakati wowote na haiwezi kuwekewa sheria. Aidha, fasihi ni kioo cha jamii na hivyo malighafi ya fasihi hutolewa kwenye mazingira halisi na hali halisi za kiuchumi, kisiasa, kisaikolojia, kijamii na hata tajriba aliyopata mwandishi kwenye mazingira yake. Zaidi ya hayo, kuwepo na kudumu kwa kazi ya kisanaa hutegemea ubunifu na upya wa aina fulani (Mohamed, 2008).

Kisawe cha komedia kwa lugha ya Kiingereza ni 'Comedy.' Neno hili linatokana na neno Komos la lugha ya Kiyunani linalomaanisha sherehe za matambiko ya jamii za watu wa Uyunani ya Kale. Katika sherehe hizo watu walifurahi kwa kuimba, kucheza ngoma na kutamba majigambo ili kumshukuru mungu wao aitwaye Dionysius ambaye ni mungu wa rutuba na mavuno (Encarta, 2007; Kennedy na Gioia, 2007: 1257). Kwa hiyo, kwa jicho la kitaaluma, komedia ni utanzu wa kidrama ambao shabaha yake kuu ni kufurahisha. Miongoni mwa sifa za msingi za utanzu huu ni ile ya utunzi na utendaji wake kuelekezwa na utendekaji wa jukwaani au mbele ya hadhira.

Kennedy na Gioia (2007) wanafafanua kuwa komedia za mwanzo kabisa zilizokuwa katika umbo lililoandikwa zilipatikana huko Uyunani katika mji wa Athens mnamo karne ya 5 Kabla ya Kristo (KK). Komedia hizo zilikuwa za Aristophanes (448-385 KK) ambaye aliziunda kwa kutumia kejeli; zilikuwa zinazungumzia masuala ya siasa za Athens, falsafa, pamoja na sanaa ya wakati huo. Katika zama hizo pia kulikuwa na komedia zilizotungwa na Menander (342-291KK) ambaye alikuwa anatoa changamoto kwa Aristophanes. Komedia za wakati huo zilikuwa zinatendeka nyakati za mchana katika kipindi cha sherehe za msimu wa baridi. Wakati komedia za Aristophanes

zilijikita katika uhalisi, zile za Menander zilikuwa kinyume chake (zilitumia mandhari na wahusika wa kubuni).

Green (1977) na Olson (2007) wanaongezea kuwa komedia zilikuwa zinafanyika jukwaani huko Syracuse katika jiji la Sicily, Uyunani, kuanzia katikati ya miaka ya 480. Huko Athens, katika miaka hiyohiyo, mashindano ya ushairi wa kikomedia yaliongezwa katika programu rasmi za kisanaa katika jiji la Dionysia mnamo mwaka 486; na takriban miongo minne baadaye, hatua kama hiyo iliafikiwa katika jiji la Lenaia. Maelezo haya ya Green na Olson yanawiana na yale ya Aristotle katika The Poetics (uk. 2), anaposema kuwa chimbuko la komedia limo katika masuala ya ‘ushairi uliopindishwa’. Hata hivyo, Aristotle anaongezea kuwa komedia haukuwa utanzu uliopewa kipaumbele kama ilivyokuwa kwa tanzia. Hii yatokana na ukweli kwamba wakati wa zama za Plato, Aristotle, na Socrates, utanzu huu ulikuwa ni wa kitabaka. Kuanzia muda huo, usanaji na utendekaji wa komedia ulienea katika jamii mbalimbali barani Ulaya na duniani kwa jumla. Matukio hayo yote yaliambatana na ucheshi au furaha iliyotokana na majigambo na tambo zilizokuwa na dhihaka na utani ndani yake. Baadaye, matukio hayo yaliingizwa katika kazi mbalimbali za fasihi andishi kama vile nathari, tamthiliya na ushairi.

Dhana ya komedia inatumiwa kama kisawe cha neno la Kiingereza ‘comic’ ambalo ni nomino inayodokeza hali. Komedia unajadiliwa kama hali ijengwayo na maneno, matendo, matukio au mazingira yoyote yenye mnato na mvuto hadi kuwafanya watu wachangamke, wafurahi, na watabasamu au wacheke. Fasili hii inatumulikia ukweli kuwa komedia hujumuisha mambo matatu kwa pamoja; mambo hayo ni ucheshi, vicheko, na furaha. Kimsingi, dhana hii ya komedia imepatikana kutokana na upanuzi wa maana-msingi ya dhana ya komedia; yaani, kijitapo cha tamthiliya ambacho hutawaliwa na u-nyemi. Kwa hiyo, komedia ni dhana inayoweza kujidhihirisha hata katika tanzu za fasihi zilizo nje ya utanzu wa tamthiliya kama

vile ushairi, nathari pamoja na Fasihi Nenwa. Dhana ya komedia imetofautishwa na ile ya komedia kwa msingi wa kwamba, komedia, kwa kiasi kikubwa, hujiegemeza zaidi katika suala la utendaji, hususan matendo ya jukwaani; ilhali, komedia huvuka mipaka ya jukwaa na kuchupa hadi katika mazingira mengine ya kimaisha kama vile katika uendeshaji wa shughuli za kiuchumi (kwa mfano, shambani, sokoni, dikoni, au bandarini), katika uandishi wa bunilizi mbalimbali, pamoja na kwenye mawasiliano ya kawaida wafanyianayo watu katika maisha yao ya kila siku.

Kutokana na utangulizi huo kuhusu komedia na komedia, mtafiti alishughulikia utafiti wake huku akichunguza mchango wa komedia za Kiswahili katika ujifunzaji na usambazaji ya Kiswahili miongoni mwa Wanafunzi wa Chuo Kikuu Cha Kitaifa cha Metropolitan jijini Mbarara hasa akiangalia komedia za Kiswahili zenye kupendwa sana na Wanafunzi hawa wa Biharwe, mchango wa komedia hizi katika ujifunzaji na usambazaji wa lugha ya kiswahili pamoja na changamoto mbalimbali zinazokumba utanzu huu wa komedia katika usambazaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa Wanafunzi wa Chuo Kikuu Cha Kitaifa cha Metropolitan jijini Mbarara.

Suala la Utafiti

Tanzu za fasihi kokote ziwapo zina mchango mkubwa katika ujifunzaji na usambazaji wa lugha hasa ya Kiswahili, lakini utanzu wa komedia umeachiliwa nyuma sana na kuangaliwa kama utanzu duni katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Badala yake, tanzu nyingine kama vile utanzu wa nyimbo, michezo, riwaya na mashairi zimeshikiliwa kuwa za muhimu katika ujifunzaji na usambazaji wa lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, utafiti huu sasa unalenga sana kuchunguza na kuchanganua mchango unaotolewa na utanzu wa komedia hasa za Kiswahili katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa Wanafunzi wa Chuo Kikuu Cha Kitaifa cha Metropolitan jijini Mbarara hasa ukizingatia ubainishaji wa komedia mbalimbali ambazo

hupendwa na Wanafunzi katika Chuo Kikuu Cha Kitaifa cha Metropolitan, kutathmini mchango wa komedia za Kiswahili katika ujifunzaji na usambazaji wa lugha ya Kiswahili na kutambua changamoto zinazokumba utanzu wa komedia katika usambazaji wa lugha ya Kiswahili.

Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na madhumuni ya utafiti yafuatayo:

- (i) Kubainisha komedia mbalimbali zinazopendwa na Wanafunzi wa Chuo Kikuu Cha Kitaifa cha Metropolitan .*
- (ii) Kutathmini mchango wa komedia za Kiswahili katika ujifunzaji na usambazaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa Wanafunzi wa Chuo Kikuu Cha Kitaifa cha Metropolitan jijini Mbarara.*
- (iii) Kutambua changamoto zinazokumba utanzu wa komedia katika usambazaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa Wanafunzi wa Chuo Kikuu Cha Kitaifa cha Metropolitan jijini Mbarara.*

Maswali ya Utafiti

Ili kufikia matokeo ya utafiti huu, mtafiti aliongozwa na maswali yafuatayo ya kiutafiti ambayo alilenga kuyapatia majibu wakati wa kutafiti kwake.

- (i) Ni komedia zipi ambazo zinapendwa na Wanafunzi wa Chuo Kikuu Cha Kitaifa cha Metropolitan ?*
- (ii) Komedia za Kiswahili zimechangiaje katika ujifunzaji na usambazaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa Wanafunzi wa Biharwe divisheni jijini Mbarara?*
- (iii) Utanzu wa komedia unakumbwa na changamoto zipi katika usambazaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa Wanafunzi wa Chuo Kikuu Cha Kitaifa cha Metropolitan jijini Mbarara?*

Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu ulimsaidia mtafiti kubainisha komedia mbali mbali ambazo zinapendwa na Wanafunzi wa Chuo Kikuu Cha Kitaifa cha Metropolitan jijini Mbarara, kutathmini mchango wa komedia katika kuendeleza na kujifunza lugha ya Kiswahili miongoni mwa Wanafunzi na pia kuchunguza changamoto mbalimbali zinazoukumba utanzu huu wa komedia katika uendelezaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

Utafiti huu pia utawasaidia watafiti wengine kwa kufanya kama nguzo watakapokuwa wanatafiti jambo linalohusiana na mada hii.

Vilevile utafiti huu utamsaidia mtafiti kupata shahada ya uzamili katika lugha ya kiswahilikwa kuwa utafiti ni mojawapo wa mahitaji ya chuo kikuu ili kupata shahada hiyo.

Nadharia ya Utafiti

Aswan B, Mayaka G, na Riro M (2018), wanakubaliana kwamba nadharia ni muhimu katika utafiti wa aina yoyote. Wanasema kuwa nadharia ni njia ya kutazama kitu katika taaluma yoyote ile. Wanasema kuwa nadharia hutoa mwongozo wakutafakari masuala maalum katika utafutaji wa maarifa kwenye taaluma mahsusi. Nadharia aliyoichagua mtafiti humpa uwezo wa kupambanua maarifa kwa misingi maalum yenye mifumo ya aina yake y pekee. Nadharia kwa mwelekeo unaokubalika kuwa na maana.

Wafula na Njogu, (2007:7) wanasema kuwa nadharia ni jumla ya maelekezo yanayomsaidia msomaji au mhakiki kuifahamu kazi ya fasihi kwa kufuata utaratibu maalumu.

TUKI, (2004:300) Nadharia ni mawazo, maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kueleza, kutatua au kutekeleza jambo fulani.

Sengo (2009), anafasili nadharia kuwa ni wazo kuu, fikira kuu, mwongozo mkuu wa mtu, watu au jamii ya pahala Fulani, wakati Fulani na kwa sababu Fulani. kwa mantiki hiyo, nadharia ni dira na mwongozo wa kulikabili jambo kifalsafa, kidini, kimantiki, kijamii na kiutamaduni.

Nadharia ya Ueneaji

Nadharia ya ueneaji kwa kiingereza inaitwa ‘diffusionism’. Nadharia hii ilichipukia huko Ufini na ina taathari zake kule Uropa. Msingi wake ni kule kuzingatia chimbuko la taaluma Fulani na kujaribu kufuata mikondo iliyopitia hadi kufikia hali ilivyo wakati wa uchambuzi. Vilevile, nadharia hii hujaribu sana kuumba upya historia ya utanzu kwa madhumuni ya kutaka kutambua hali na aina yak kwanza kabisa ya fani hiyo. Mbinu inayotumiwa ni kutafuta viashiria vya fani hiyo ili kuainisha chimbuko lake.

Imani ya wanaueneaji ni kwamba fasihi simulizi haibadilishi hadhi yake bali huenea. Hadithi, kwa mfano, ikipata misingi thabiti, huweza kuenea kokote bila kuzuiliwa na chochote na pia hudumu kwa muda mrefu. Aidha, maudhui yake ya kimsingi hudumu lakini muundo huweza kubadilika kulingana na mazingira.

Wataalamu hawa wa Ufini walishikilia kuwa fasihi huweza kupenya kuta za kikabila. Walijaribu kuthibitisha kuwa fasihi simulizi huzagaa zaidi kutoka jamii zilizoendelea kuelekea jamii za kishenzi. Ithibati waliyotoa ni kwamba hadithi za kizungu zinapatikana kwa wingi miongoni mwa wa Wamarekani asili na Waafrika.

Pia, wanadai kuwa ni nadra kupata hadithi za jamii hizi (jamii za kishenzi/duni) miongoni mwa jamii zilizostaarabika au watu waliostaarabika. Hata hivyo, hao walisahau kuwa jamii hizi zilichukua hatua za kukandamiza tamaduni za watawaliwa na hivyo kupuuza fasihi yao. Hawangeweza kuthamini Sanaa ya ‘washenzi’ kwa vile tayari waliaminii kuwa wenyeji walikuwa wajinga. Waliadini kwamba fasihi simulizi,

kama vile fasihi andishi, zilibuniwa wakati Fulani na mtu mmoja na baadaye ikaenea kotekote katika jamii. Inadhihirika basi kuwa ueneaji hujikita sana katika kutafuta msingi au chimbuko la utanzu wowote ule.

Upungufu wa nadharia hii, ni kwamba ni vigumu kwa mtafiti kukusanya visawe vyote vya hadithi kwa madhumuni ya kuvianisha. Hii ni kwa sababu watu hutegemea watu wanaoishi na labda hadithi chache zilizoandikwa kama data.

Upungufu mwingine wa nadharia hii ya ueneaji ni kule kukiuka umuhimu wa fasihi katika jamii mamboleo na kuhimiza zaidi asili ya fasihi hiyo. Aidha, nadharia hii hupuuza dhima ya fanani katika kuendeleza fasihi simulizi.

MBINU ZA UTAFITI

Utangulizi

Sura hii inaeleza mbinu zilizotumiwa katika utafiti huu. Ni sura ilijumuisha mpango wa utafiti, jumuiya ya utafiti, eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, vifaa ya utafiti, mbinu za ukusanyaji data na uchanganuzi wake iliyopatwa nyanjani, utaratibu wa utafiti, na vikwazo vilivyojitokeza katika utafiti huu.

Mpango wa Utafiti

Mtafiti alitumia muundo wa uchunguzi kimaelezo. Muundo huu hukadiria matokeo kitakwimu na baadaye maelezo na tathmini hutolewa. Waaidha, hueleza na kufafanua matukio kama yalivyo, yalivyokuwa au yatakavyokuwa (Kombo & Tromp, 2006). Utafiti huu ulitumia hojaji, mahojiano na majadiliano. Hii ilimwezesha mtafiti kupata maarifa yote kuhusu mchango wa komedia za Kiswahili katika uendelezaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa Wanafunzi wa Chuo Kikuu Cha Kitaifa cha Metropolitan jijini Mbarara.

Eneo la Utafiti

Kabla ya kukusanya data za utafiti ni jambo muhimu sana kuchagua mahali ambapo yatakusaidia kupata taarifa inayoutosha utafiti. Eneo la utafiti lilikuwa ni jamii ya Chuo Kikuu cha Metropolitan inayopatikana katika Chuo Kikuu Cha Kitaifa cha Metropolitan jijini Mbarara kwenye barabara la Mbarara-Masaka baada ya Kasingenge.

Sampuli Lengwa

Walliman (2011), anafafanua kundi lengwa kuwa ni jumla ya vitu vyote vinavyohusika katika utafiti (vinavyotafitiwa) yaani watu, taasisi, vitu au matukio. Kwa ujumla, kundi lengwa ni jumla ya walengwa wote wa utafiti ambapo sampuli inaweza kuchaguliwa. Kothari (2004:55), anaelezea kuwa, uteuzi wa walengwa ni mbinu au utaratibu ambao mtafiti atatumia katika kuchagua orodha ya vitu au watu kwa ajili ya sampuli. Katika utafiti huu kundi lengwa la utafiti huu lilikuwa ni wanafunzi, wahadhiri pamoja na wapenzi wa Kiswahili kutoka chuo kikuu Metropolitan, kwa sababu mtafiti aliwakisia kuwa wanauwezo na kuelewa jinsi komedia za Kiswahili zinavyokuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili.

Sampuli na Usampulishaji

Babbie (1992), anasema kwamba, sampuli ni sehemu ya idadi ya watu ambayo mtafiti anavutiwa nayo katika kupata taarifa na kutoa hitimisho la utafiti wake. Katika utafiti huu wasailiwa 50 waliteuliwa kwa kutumia usampulishaji lengwa. Miongoni mwao, wasailiwa 04 walikuwa wahadhiri wa Chuo Kikuu Metropolitan wanaofundisha lugha ya Kiswahili na fasihi yake. Wasailiwa 35 walikuwa wanafunzi wa Metropolitan ambao walikuwa wanafunzi wa lugha ya Kiswahili na fasihi yake. Wasailiwa 11, walikuwa ni wapenzi wa Kiswahili ambao walipatikana Chuoni Metropolitan lakini

kwao hawakuwa wanafunzi wa Kiswahili wala wahadhiri wa Kiswahili. Mtafiti aliamua kutumia aina hizi za sampuli katika utafiti wake kwa sababu aliamini kuwa makundi hayo ndiyo yalikuwa na uwezo wa kutoa taarifa faafu kuhusiana na malengo pamoja na maswali ya utafiti huu.

Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Kothari (1990), anasema kwamba ukusanyaji data ni zoezi la awali katika utafiti ambalo humwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kumfikisha kwenye malengo yake ya utafiti. Vilevile, Kothari, anaendelea kusema kuwa hatua ya uwasilishaji na uchanganuzi wa data haiwezi kufanyika kabla ya hatua hii ya ukusanyaji data. Msaghaa (2010) anasisitiza kuhakikisha kuwa mbinu za utafiti zinatoa aina ya taarifa zinazohitajika kujibu swali la utafiti. Mtafiti alitumia mbinu ya hojaji, mahojiano, na majadiliano. Mbinu hizi zilimsadia sana mtafiti wakati wa kukusanya data ya utafiti wake kuhusu mchango wa komedia za Kiswahili katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa Wanafunzi wa Chuo Kikuu Cha Kitaifa cha Metropolitan, jijini Mbarara.

Mahojiano

Mahojiano yalifanywa baina ya mtafiti na wahojiwa. Mbinu hii ilihusisha uwasilishaji wa maswali kwa wasailiwa/wasailiwa wa maswali hayo ambayo yalijibiwa kwa njia ya mdomo na mtafiti alikuwa akiyaandika majibu hayo katika shajara yake.

Mbinu hii ni ya madhubuti katika kumpatia Mtafiti data za kutosha kujibu maswali ya utafiti wake kwa muda mfupi. (Borg na Gall, 2003). Kothari, anaendelea kusema kuwa mbinu hii inaruhusu mtafiti kuuliza maswali ya ziada. Mbinu hii ilimwezesha Mtafiti kupata data ambazo hapo awali hakutegemea kuzipata. Aidha, mbinu hii ilimwezesha mtafiti kuuliza maswali ya ziada na kufafanua ipasavyo maswali ambayo

hayakueleweka kwa wasailiwa. Vilevile, baadhi ya wahojiwa walipata nafasi ya kufafanua majibu yao na kumtaka mtafiti kuyaweka wazi baadhi ya maswali ambayo hayakueleweka ipasavyo kwao.

Mbinu ya Hojaji

Mbinu hii ya hojaji ni mbinu ya utafiti ambayo kwayo mtafiti huandaa maswali kuhusiana na jambo fulani. Maswali hayo yanaweza kuhitaji majibu marefu au mafupi kutegemeana na taarifa inayohitajika na mtu anayepewa maswali hayo. Katika utafiti huu, mbinu hii ilisaidia katika kukusanya data ambazo mtafiti alizipata kutoka kwa wanafunzi, wahadhiri na vipenzi wa Kiswahili chuoni Metropolitan . Mbinu hii ilimsaidia mtafiti kukusanya data kwani aliwapatia maswali wahojiwa katika maeneo yao kulingana na malengo ya utafiti. Mbinu hii ilimwezesha Mtafiti kukusanya data nyingi kwa muda mfupi kutoka kwa wasailiwa wengi tofauti kama ilivyokuwa katika mbinu ya usaili. Ilimwezesha Mtafiti kutumia muda wake vizuri kwani wakati wasailiwa walipokuwa wakijaza hojaji, yeye alikuwa akiendelea na shughuli nyingine za utafiti kama upangaji wa baadhi ya matokeo.

Mbinu ya Majadiliano

Kwa mujibu wa TATAKI (2013), Majadiliano, ni mazungumzo ya watu wawili au zaidi wanaobadilishana mawazo kuhusu mada fulani. Njia hii ilitoa nafasi kwa Mtafiti na mtafitiwa kubadilishana mawazo. Hivyo ilisaidia mhojiwa kutoa haraka taarifa na habari nyingi nzuri zilizofaa utafiti huu.

Vifaa vilivyotumika katika Utafiti

Mtafiti aliandaa vifaa vya utafiti kulingana na mada na malengo ya utafiti. Vifaa hivi vilimwezesha mtafiti kukusanya data na kupata taarifa sahihi za utafiti wake. Vifaa

hivi vilikuwa, mwongozo wa mahojiano, mwongozo wa majadiliano pamoja na hojaji. Vifaa hivi vilitumiwa kukusanya data iliyoufaa utafiti huu pamoja na malengo yake.

Mwongozo wa Mahojiano

Kifa hiki kilitumiwa kukusanya data ya msingi kwa kuunda maswali yaliyolizwa kwa wasailiwa ambao waliyajibu barabara na mtafiti alikuwa akiandika maoni yao katika daftali yake. Baada ya kuandika maoni hayo, alikuwa akiyarudia tena ili kuyachuja na kuibuka na data faafu kwa ajiri ya malengo na maswali ya utafiti wake. Kifaa hiki kilimsaidia mtafiti hapo mwanzoni kabla ya kufungwa (baada ya uambikizi wa virusi vya korona), kwa sababu alikutana na wanafunzi wa Chuo Kikuu Metropolitan na kuwauliza uliza kuhusu maswali yake ya utafiti. Kilimsaidia kupata mawazo yao kuhusu mchango wa komedia za Kiswahili katika ujifunzaji na usambazaji wa lugha ya Kiswahili kwa Wanafunzi wa Biharwe .

Hojaji

Hii ni mbinu ambayo mtafiti alitumia katika ukusanyaji wa data ya utafiti kutoka nyanjani. Mtafiti aliunda maswali kadhaa yenye uhusiano na mada ya utafiti; shabaha na maswali yake ya utafiti. Kulikuwa na maswali ambayo yaliandikwa kwa matumizi ya tarakirishi na kunakilishwa kwa karatasi na kuchukuliwa kwa wanafunzi, wahadhiri na wapenzi wa Kiswahili Chuoni Metropolitan . Hawa walijibu maswali hayo na baadaye mtafiti aliyapokea majibu yao na kuyachunguza kama inavyoonyeshwa katika sura ya nne ya utafiti huu.

Utaratibu wa utafiti

Mtafiti alitoa barua ya utambulisho kutoka kwa mkuu wa kitivo cha isimu na sayansi za jamii Chuo Kikuu cha Kiislamu kilichopo nchini Uganda; ambayo ilimwezesha

kukubaliwa kufanya utafiti wake katika jamii ya Metropolitan Chuo Kikuu Cha Kitaifa cha Metropolitan , jijini Mbarara.

Uwasilishaji na Uchanganuzi wa data

Mtafiti alipanga na kuchambua moja kwa moja data aliyoipata kutoka nyanjani kwa wasailiwa na kuichambua ili aiorodheshe na iwe taratibu halafu akatoe rai jumuishi ya msimamo kuhusu Mchango wa komedia za Kiswahili katika ujifunzaji na usambazaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa Wanafunzi waBiharwe jijini Mbarara.

Vizuizi vya Utafiti

Mtafiti alikumbwa na vizuizi vifuatavyo wakati wa kukusanya data ya utafiti wake: Uchelewaji wa hojaji kutoka kwa wasailiwa uliosababishwa na janga la uambukiza wa virusi vya Korona uliowafanya wanafunzi wote wa Chuo Kikuu Metropolitan kwenda nyumbani. Suala hili lilimchelewesha katika mipango yake ya kutafiti na kupangilia matokeo yake ya utafiti. Mtafiti alisuluhisha hili tatizo kwa kuwasiliana na wasailiwa wake walipokuwa nyumbani na kutumia mitandao ya kijamii wakati wa kukusanya data. Gharama kubwa aliyoitumia wakati wa kuwasiliana na wasailiwa wake kupitia kwa mitandao ya kijamii, wakati walipokwenda nyumbani kwa sababu ya janga la Virusi vya Korona. Kizuizi hiki kilimtatiza mtafiti kwani ilimbidi awasiliane nao na baadhi yao walikuwa wakimwambia kuwa hawakuwa na uwezo wa mtandao na kumbidi yeye mwenyewe awanunulie data ili wawasiliane na apate maoni yao kuhusu malengo na maswali ya utafiti wake. Kizuizi hiki kilitatuliwa na mtafiti mwenyewe kwa kuomba mkopo kwa watu wa familia yake ili umsaidie kugharamia malipo yote yaliyojitokeza katika shughuli yake ya utafiti. Ufungwaji wa Chuo ulimtatiza mtafiti kwani, alikosa nafasi ya kupata data ya upili ambayo alikuwa anatarajia kuipata

maktabani na kuitumia kama nyenzo ya kupimia matokeo yake ya utafiti huu kuhusu mchango wa komedia za Kiswahili katika ujifunzaji na usambazaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa Wanafunzi wa tarafa ya Biharwe , jijini Mbarara. Hili lilitatuliwa kwa matumizi ya tovuti pamoja na mitandao ya kijamii ili kupata data ya kupimia matokeo ya utafiti huu.

MAREJEO

Aswan B, Mayaka G, na Riro M (2018), misingi ya nadharia za utafiti: Serengeti book sells. Nairobi.

Cohen, A. (2000), *Research Methods in Education*. London: Routledge Falmer.

Songoyi, (2005). *Tasnifu juu ya Miundo na Maudhui ya nyimbo za Kisukuma*.

Fadhili, E. F. (2014). *Dhima ya mtindo katika tamthilia za kihistoria. Utafiti linganishi wa*

Habwe na Karanja, (2004), maendeleo ya lugha pamoja na asili yake. Nairobi: Focus Publisher.

Kezilahabi, E. (1976). *“Ushairi wa Shaaban Robert”*. Nairobi: East African Literature

Bureau. Kiango, S. D. (1980). *“Tamthiliya ya Kiswahili na Mabadiliko ya Dhamira*

1957. 1975” Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Ltd.

Mulokozi, M. (1996), *Fasihi ya Kiswahili, Dar es salaam. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.*

Publishers.

Satu, E. na Helvi, K. (2007). *The Qualitative Content Analysis. Janual of Research Methodology.*

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi. Dar es Salaam: KAUTTU Limited.*

tamthilia za Morani na Kinjekitile. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahil Sanifu. Dar es salaam. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.*

TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu. (Toleo la 2). Nairobi: Oxford University Press.*

TUKI, (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Nairobi; Oxford University Press.*

Wafula, R. M na Njogu, K (2007). *Nadharia za uhakiki wa Fasihi. Sai Industries Ltd. Nairobi.*

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake. Nairobi: Phoenix Publishers.*

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi. Nairobi: Focus Publisher.* Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia. Focus Publication Ltd. Nairobi Kenya.*

Wamitila, K. W. (2008). *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi. Nairobi: Nairobi: Vide Muwa.*

Wamitila, K. W.(2002). Uhakikiwa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake. Nairobi:

Phoenix

Wamitila, K.W. (2003). Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia. Nairobi: Focus

Publications

Wamitila, K.W. (2010). Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi. Nairobi:

Vide Muwa.